# *BARUA #01; MAANA YA MAFANIKIO KWAKO.*

Rafiki yangu mpendwa,

Mafanikio yana maana tofauti kwa watu tofauti.

Ndiyo maana mara zote nimekuwa nasisitiza usishindane na mtu yeyote yule, kwa sababu mbio mnazokimbia zinatofautiana kabisa.

Usipojua maana ya mafanikio kwako, utajikuta kila wakati unatangatanga na usijue kipi cha kusimamia. Unaweza kushindana na watu na ukashinda, lakini bado ndani yako ukawa na utupu.

Kutokuwa na maana ya mafanikio imekuwa chanzo cha wengi kukimbizana na kila aina ya fursa mpya kitu kinachowapelekea kujaribu mambo mengi na kushindwa kufanikiwa.

Moja ya maswali ambayo nilikuomba ujibu kwenye mwongozo wa mwaka wa mafanikio

2020/2021 ni maana ya mafanikio kwako na unajipimaje umefanikiwa.

Nimepata majibu mazuri na ya tofauti kutoka kwa kila aliyejibu.

Hapa nimekusanya majibu yote kama ambavyo kila mtu aliandika, ili iwe sehemu ya kufanya rejea kwa kila mmoja wetu, kuepuka kuhangaika na mambo yasiyokuwa na mchango wa kutufikisha kule tunakotaka kufika.

Karibu usome maana ya mafanikio na jinsi ya kujipima kimafanikio kama ambavyo kila mwanamafanikio ameeleza.

# MAANA YA MAFANIKIO NA JINSI YA KUJIPIMA

Mafanikio kwangu maana yake ni kuwa huru kifedha huku nikiwa na afya njema ya kimwili, kiroho na kimahusiano. – Simeon Shimbe

Mafanikio kwangu yana maana ya kujua kusudi langu hapa duniani kuliishi kusudi hilo kutoa mchango wangu katika kuwasaidia watu wengi zaidi wapate wanavyovitaka. Hiyo ndio maana

ya mafanikio kwangu. Kigezo ninachotumia kupima mafanikio yangu ni kujiimarisha kila siku kwenye sehemu kuu tatu akili, mwili na roho. Maisha yangu yakiimarika kwenye maeneo matano yaani akili, mwili roho, mahusiano, fedha na kazi ndiyo nitajihesabu imefanikiwa. - Ernest Theobald Paschal

Mafanikio kwangu ni kutoka kwenye ajira na kujitegemea, watoto wangu kufikia elimu kiwango cha digrii, kuwa na uhuru wa kifedha kwa kuacha kulalamika kuhusu fedha ya kutumia mahitaji ya lazima. – Sebastian Kalugulu

Mafanikio kwangu ni Uhuru wa kipato kutoka biashara na uwekezaji bila mimi kufanyia kazi fedha. Niwe na afya bora na familia inayosikilizana lakini wanafamilia wasiwe tegemezi. - Godfrey Mathias Mbise.

Maana ya mafanikio kwangu: Ni kutimiza kusudi la maisha yangu ambalo ni kusaidia watu wengi kuondokana na ujinga na maradhi; ambavyo ndiyo chanzo kikuu cha umasikini.

Kigezo ninachotumia kupima mafanikio yangu ni pale ambapo watu wengi watatumia na kusaidika na kazi zangu za kisayansi na uandishi. - Felician Clement Meza

Kwangu mafanikio yana maana ya kufikia lengo lako. Maisha yangu yakifikia hali ya kuwa na biashara itakayokuwa na uwezo wa kujiendesha yenyewe hata kama sipo, na kutengeneza Akiba ambayo itatosheleza kuendesha maisha yangu na familia kwa miaka mitano mbele haya kwangu yatakuwa mafanikio makubwa. - Flora Sanze Mulishi

Mafanikio yana maana kubwa kwangu hasa pale yanapo pitia kwenye mchakato unao leta matokeo chanya kwangu na kwa wale wanaonizunguka. Kigezo ninacho tumia kupima mafanikio yangu ni pale ninapo badilisha kisicho kuwa na ufanisi na kuwa na ufanisi na msaada kwa jamii inayonizunguka, mfano, nilinunua fukwe iliyo wazi na sasa imeendelezwa na kuwa kiwanda cha kuzalisha madini chumvi na kinatoa ajira kwa jamii na kuleta maendeleo kwangu au nimenunua pori na kulifanya kuwa

shamba La mikorosho na kuanza kuvuna mikorosho. Maisha yangu yakiwa yanaendesha miradi na viwanda vinavyo zalisha matokeo chanya kwangu na kwa jamii inayonizunguka hayo ni maisha mafanikio makubwa sana kwangu. - Freddy Mwizalubi Ndolezi

Kwangu mimi naamini Mafanikio ni  Kuwa huru kufanya kile kitu unachopenda kufanya huku ukiwa pia na  furaha muda wote unapofanya kitu hicho. Vigezo ninavyotumia kupima mafanikio yangu. Nina uhuru kiasi gani wa kufanya vile vitu ninavyopenda kufanya hata kama siingizi kipato. Nina furaha kiasi gani katika kutimiza majukumu yangu. - Mahule Peter.

Mafanikio kwangu maana yake ni katika kazi, kufanya kazi kwa ubora na kupata matokeo mazuri au yenye kuleta matumaini, na katika biashara nikitoa huduma bora kwa mteja akaridhika hiyo nahesabu Kama mafanikio kwangu.  - Basil Danghalo Allay

Mafanikio kwangu ni kule kuweza kuwa na majibu ya kwa nini ninaishi, ninakwenda wapi na ninahitaji nini kufika pale ninapo taka kufika. Nitahisi kuwa nimefanikiwa pale ninapoweza kujijua fika mimi ni nani, ninataka nini, na ninavyoweza kukabiliana na mahitaji yangu muhimu na ya familia yangu. - Palmo Israel Ulomi

Mafanikio kwangu na yatafasiri kwamba ni juhudi kubwa na sahihi + hatua sahihi = matokeo sahihi ambayo yanazalisha mafanikio makubwa zaidi.  Kigezo ninacho tumia kupima mafanikio kwangu ni ile hali ambayo ninaishi kwa amani na jamii yangu, afya njema, kuishi MAISHA ambayo hayaandamwi na madeni, pamoja na mikopo. Ninajihesabu kwamba nimefanikiwa pale  ninapochukua hatua sahihi nakutoa matokeo sahihi niliyodhamiria kuzalisha. - Emanuel marwa maitarya

Maana ya mafanikio: Amani, afya nzuri, mahusiano mema, uhuru wa kifedha na kufanya niyapendayo. - Stanslaus P. Kashinje

Kwangu mimi mafanikio ni pale nitakapoweza kufikia yale ambayo hasa ni ndoto na kiu yangu kuyafikia hapo nitakua nimefanikiwa. Lakini pia nikiweza kugusa maisha ya mtu walau mmoja kwa kile ninachokifanya na kikamwezesha naye kupiga hatua fulani kwangu mimi ni mafanikio. Mfano nikiweza kuandika jambo na likamsaidia mtu najiona nimefanikiwa, nikiwa na wafanyakazi na nikaweza kuwalipa na wakaridhika na mazingira ya kazi kwangu mimi hayo ni mafanikio. - Elizabeth Stephen Mgheni

Maana ya mafanikio kwangu ni kufikia ushindi na kuweza kusaidia jamii kwa matokeo niliofikia kwa HEKIMA. Kigezo cha kupima ni kuweza kuzalisha watu  wanaoweza kuwa kama Mimi niliofikia mafanikio kunipita niliofikia. - Christopher Mwijage

Kwangu mimi mafanikio yana maana kugusa Maisha ya wengine kwa kutoa thamani Zaidi kwao. - Innocent Didas Kavishe

Mafanikio kwangu ni kutimiza ndoto zangu (niwe na biashara zinazojiendesha in my

absence) na kuishi maisha ya uhuru . Niwe na uwekezaji pia kwenye ardhi, majengo, hisa makampuni mbalimbali, hati fungani etc - Xhenniah Kiwango

Mafanikio kwangu ni kuwa na amani, furaha na uelekeo juu ya maisha yangu, maisha yangu yakiwa yapo kwenye mwelekeo wa lengo nililojiwekea ndio nayaona mafanikio pia - Notbruga Basili

Mafanikio katika maisha wakati mwingine sio vitu ulivyonavyo au unavyomiliki, bali uwezo wako wa kukabiliana na changamoto na namna unavyoweza kuzitatua, mimi kwa kiasi fulani kupitia Maarifa ya kisima cha Maarifa nimeweza hilo kutatua changamoto ya kindoa/mahusiano. Pia tarehe 07/11/2020 nilipofunga ndoa, maandalizi yake na kufikia hatua nimejifunza mengi hasa ukizingatia nilikuwa narudia kufunga ndoa kwa mara ya pili, nilipata matokeo au kupokelewa vizuri FUNDISHO KUU,KTK MAISHA HATUPASWI KUKATA TAMAA,BILA KUJALI NI CHANGAMOTO KUBWA KIASI GANI TUNAPITIA UWEZEKANO

WA KUJENGA UPYA MAISHA YAKO UPO NA NI MKUBWA, MUHIMU NI KIJITHAMINI. - Beatus Elias Rwitana

Mafanikio kwangu ni kuwa huru kifedha na kujali wengine. - Yusuph I. Yusuph

Kigezo ambacho nitatumia Kama nimefanikiwa ni pale ambapo nitakuwa na uwezo wakuingiza fedha inayokidhi mahitaji yangu na familia bila kuhusika moja kwa moja yaani hata kama nikiwa nimelala niwe na uhakika fedha IPO - Bosco victor mlomo

Mafanikio kwa upande wangu ni kugusa maisha ya watu na kuyafanya kuwa bora kupitia shughuli zangu ninazofanya. Kuwapatia elimu juu ya umuhimu wa matunda na kuwaandalia matunda na kuimarisha afya. Kigezo ninachotumia kupima mafanikio ni kuona watu wananufaika kupitia ninachokifanya na afya yao inaimarika. - Mustapha Kunyaula

Mafanikio kwangu yana maana nikitimiza lengo langu kuu kwa chochote ninacho panga kufanya nikikitimiza hapo tayari nimefanikiwa.

Kigezo ninacho pima kupima mafanikio yangu ni kuangalia hatua kidogokidogo ninayo piga kila siku. Kwenye maisha yangu nikiwa na biashara kubwa ama mmiliki wa kampuni, gari nzuri yakutembelea nyumba nzuri ya kifahari hapo najihesabu mtu ambaye amefanikiwa. - Kizito bakwanye masereka

Mafanikio yana maana ya kutoa huduma bora kwa wateja kwa mahitaji ambayo wanahitaji kwenye maisha yao, kipimo ambacho najipima report yangu ya mwezi kuanzia mapato, matumizi, uwekezaji, nidhamu kwenye biashara yangu. - Mary Charles Kunena

Ninapowawezesha wengine kuweza kujitegemea na kufanikiwa ndipo ninapoona maisha yangu yana maana. Ninapima kwa kuangalia idadi ya watu wanaofanikiwa kupitia mimi. Nitakapokuwa na uwezo wa kujitegemea na kubadilisha maisha na mitazamo ya watu wengi zaidi - Moses Mahenge

Kwangu mafanikio ninapima kwa kuweza kutatua changamoto nyingi zaidi ndio mafanikio yangu. - Wade Pius Kibadu

Maana yake kufikia lengo ulilоweka, kigezo ni kuanza na kuendelea kufanya hata kama ni kidogo kidogo bila kukata tamaa. Nitakuwa nimefanikiwa pale ambapo nitaendelea bila kuacha. - Huvira Hezron Konga

Maana ya mafanikio kwangu ni kitendo cha kuwa nimefanikiwa katika mambo yafuatayo; Kiroho/ moyoni kuwa na amani na furaha ktk maisha. Kiakili - kila siku kuendelea kujifunza na kutumia yale ninayojifunza. Kimwili - kuwa na afya njema. - Regina Panga

Maana ya mafanikio kwa tafsiri yangu ni kutimiza au kufikia makusudi yale ambayo nililetwa kufanya hapa duniani. Kigezo kikuu cha kunifanya niseme nimefanikiwa ni; Kuwa na ufahamu juu ya sababu ya mimi kuwepo hapa duniani. Kutekeleza kwa vitendo majukumu ambayo nimepanga kuyafanya kila siku – Isaack Zake

Mafanikio yana maana kuwa huru ya kufanya kile ninachoweza kufanya kwa wakati wowote ambayo kina manufaa kwa wengine na kwangu pia. Kigezo nitakachotumia kupima maisha yangu kila siku kuwa tofauti na siku iliyopita. Nikiwa Uhuru kifedha na muda na kila kitu nitajihesabu nimefanikiwa. - Patrick Edgar James

Maana ya mafanikio kwangu: 1.Uwezo wa kujithibiti. Kubaki kuwa, wakati wengine wanapokuwa na maoni tofauti. 2. Mafanikio yangu unapokuwa mwanga na chachu kwa wengine - Alfred Mwanyika

Mafanikio yana maana ya mimi kuweza kuishi na kuitimiza ndoto kuu ya maisha yangu. Nitajihesabia kuwa nimefanikiwa ikiwa nitaweza kutimiza na kuishi maisha ya ndoto yangu. - Donard Msanga

Maana ya mafanikio kwenye maisha yangu; ✓ Kuwahudumia watu wengi zaidi kupitia shughuli ninazofanya katika kutatua changamoto zao. ✓ Kuwa huru kuishi maisha ninayoyataka bila

kuhofia chochote. ✓ Kutumia vipaji nilivyonavyo Kuwasaidia wengine. - Tumaini Jonas Anthony

Mafanikio yana maana yakuwa huru na kuwa na furaha na kuweza kumudu chochote ninachohitaji, napima mafanikio yangu kwa jinsi ninavyoweza kutatua matatizo yanayojitokeza kila siku katika maisha yangu. - Deogratius Kiangu

Mafanikio kwangu ni kuwa BORA ZAIDI YA JANA. - Ghati Ndare Mairo

Mafanikio yangu yana maana kubwa sana, kwanza nafanya kitu ambacho napenda sana, pia napenda kusaidia wengine nao wapige hatua. Kigezo ambacho natumia kupima mafanikio yangu nipale nitakapokuwa na uhuru wa kifedha na utoshelevu. - Ashiri Hamisi Mapunda

Kwenye suala LA mafanikio  yangu ni kuona nakuwa na Uhuru Wa kifedha, yaani pesa inifanyie kazi Mimi na siyo Mimi niifanyie kazi ili nilipwe Bali nataka kuona pesa naweka mahala

na kuhakikisha inafanyia kazi vile ninavyotaka Mimi na hii si kazi rahisi, Ila lazima nijitoe na pia kufanya vitu tofauti ili kuleta matokeo tofauti kabisa na kuweza kusonga mbele haswa upande  Wa kifedha, kwa kuwekeza sehemu tofauti tofauti pia - Faustine b Buyamba

Mafanikio yangu nayapima pale nitakapoweza kufikia uhuru wa kifedha. Hivyo nitakapofikia uhuru wa kifedha ndio nitajiona nimefanikiwa. - Ali Khamis

Mafanikio yana maana ya kwamba kuwasaidia watu wengine katika kila shughuli ninayoifanya ili Mungu atukuzwe kupitia mafanikio nitakayoyapata mimi. Hadi nitakapoona watu wengine wanamsifu Mungu kupitia kazi zangu na mafanikio yangu. - Elia Jacob Hassani

Mafanikio kwangu ni uhuru; uhuru wa kipato, uhuru wa muda, uhuru wa kufika sehemu mbalimbali. Pale kipato kitakapokuwa sio kikwazo tena kwa mimi kununua ninachokitaka, kufanya kile ninachokitaka au kufika  sehemu ninayotaka kufika, hapo nitakuwa

nimefanikiwa, ni kama vile unaumwa huku una bima ya afya, hauhofii ukifika hospitali unatibiwaje. - Reinfrid Martin Maganga

Mafanikio kwangu yana maana kupiga hatua na kuwa na uchumi imara, afya bora, familia yenye furaha na imani ya kiroho kuwa safi kwa kufanya ibada kuwa karibu na mungu muda wote, kuwa na uwezo wa kusaidia wenye shida katika jamii. Kigezo cha mafanikio yangu ni kuwa na uwezo wa niliyoyataja hapo juu kuyafanikisha. - Mwene Khalifa

MAANA YA MAFANIKIO KWANGU: Kufikia uhuru wa kifedha (billionea - liquidity), kuwa na mahusiano yaliyo imara, kuwa na utulivu wa ndani, afya bora na kunufaisha wengine kupitia Maisha yangu. Nayapima mafanikio kwa mzunguko wa fedha, utulivu wangu wa ndani na namna ninapo kabiliana na changamoto mbalimbali za kila siku kutathmini hatua ndogondogo za kila siku kuelea kuwa bora Zaidi. - Deodatus A Kessy

Mafanikio kwa mtazamo wangu ni kitu ninachokipenda na ninapopanga kuweza kufikia kama nilivyopanga au karibia na kufikia lengo langu. Na mafanikio kwangu siyo eneo la kifedha tu, bali ni maeneo mengi yanayohusisha mwili akili na roho ndiyo utatu wa mafanikio. Ninavyopima mafanikio mimi si kwa kuangalia wengine wana nini ambacho sina, bali ni hatua gani niliyoweza kuifikia  kwa malengo niliyokua nayo na kulinganisha nilivyo leo na jana yangu katika eneo husika nililokua nimejiwekea. - Hendry Stuart Lema

Mafanikio kwangu ni kufikia lile kusudi nililojiwekea katika maisha yangu. Kuwa mjasiriamali na mwekezaji na kuweza kutoa mchango katika maendeleo ya taifa langu. - Raphael Macha

Najihesabu  kuwa nimefanikiwa pale ambapo nimefikia malengo niliyojiwekea, kuwa na uhuru wa kifedha  na pia kuisaidia jamii inayonizunguka kwa hali na Mali pia Nina Ndoto ya kuwawezesha wale waishio katika mazingira magumu - William Loma Gurty

Mafanikio kwangu ni hali ambayo mtu anakuwa amefikia baada ya kukamilisha malengo yake ambayo alikuwa amejiwekea katika maisha yake. Kigezo ninachotumia kupima mafanikio yangu ni kuona nimekamilisha malengo yangu mbalimbali ambayo nimeyaweka. Maisha yangu yakiwa yenye uhuru kiuchumi, kiafya na kijamii ndipo najihesabu nimefanikiwa. - Fabian Philimon Hinju

Maana ya mafanikio kwangu ni kugusa jamii kwa kila jambo ninalofanya - Frank Mapunda

Mafanikio yana maana kubwa kwangu kuwa ni kuwa na uwezo na nguvu ya kifedha kuweza kutatua matatizo yangu na ya wengine bila stress. Maisha yangu yakiwa na uwezo wa mkubwa wa kifedha, kiafya, kififikra na uwezo wa kuwainua wengine nitahesabu nimefanikiwa. - Sarah Reuben Losaru

Kufikia uhuru wa kifedha, kuwa na uhuru na muda wangu, nikiweza kupata pesa hata kama nimelala. - Symphorose James

Mafanikio, kwangu yana maana ya kuwa na uwezo wa kukidhi hitaji lolote wakati wowote. - Alex Edward

Mafanikio kwangu yana maana ya kupata kile ninachotaka. Nitajiona nimefanikiwa nitakapotimiza ndoto yangu. - Nyakibengei Mugomba

Maana ya mafanikio kwangu ni kuwa na utoshelevu na ubora katika maeneo muhimu sita; (1)Afya bora kiroho/Kiimani. (2)Afya bora kiakili – Maarifa/hekima. (3)Afya bora kimwili. (4)Afya bora kimahusiano mke, watoto/wazazi, ndugu wa kuzaliwa na watu wengine ikiwepo wateja, wafanyakazi na waajiri. (5)Afya bora kisaikolojia (mtazamo chanya ktk mambo yote). (6)Afya bora kiuchumi – kuwa na ukwasi endelevu ambao unatumika kwa haki na dunia kuufurahia. - Christian Shoo

Mafanikio yangu yana maana kwanza kwa Familia yangu ndugu na jamii ninayoizunguka. Tunapima pale mtu anapokuwa ameweza kuwa na uhuru huo. - Dickson paulo mollel

Mafanikio yana maana ni uhuru kamili - Elihuruma Malack Nnko

Mafanikio kwangu ni kuwa vyema/Sawa kwenye maeneo haya matano; a/ Afya ya mwili na akili. b/Elimu na hekima. c/Kazi yenye ufanisi wa kiwango kipya kila leo. d/Fedha zinazotosha na kuongezeka. e/Mahusiano thabiti kuanzia mimi mwenyewe (Roho, mwili na akili) na kuwagusa kwa uchanya wote wanaonizunguka kuanzia ngazi ya familia hadi dunia. - John Magori Matiku

Kwangu mafanikio yangu nayapima kwa kuhakikisha wanaonizunguka wanafanikiwa kupitia maarifa kama ambavyo mimi ninakwenda kufikia mafanikio ya juu, nitajitahidi kuendelea kuandika ili kuwaokoa wengi na mtazamo hasi wa mafanikio na kuifanya jamii ya Kitanzania kuwa bora kabisa. Shida zote na mahangaiko ya watu hutokana na fikra potofu kuhusu mafanikio. – Kelvin Kinyaga

Maana ya mafanikio kwa upande wangu ni pale ninapoweza kupiga hatua ya kusonga mbele

kuelekea malengo niliyojiwekea katika jambo lolote, hasa kuwa bora kila mara kuliko nilipo sasa. Mafanikio yangu huwa nikiyapima kwa kutazama hatua za kusonga mbele nilizoweza kupiga kuelekea malengo yangu nikilinganisha na pale nilipo kuwa. Kuweza kujisimamia katika mambo yote muhimu. – Alex Kamata

Maana ya Mafanikio kwangu ni kutimiza malengo niliyojiwekea na kupata matokeo mazuri. Sasa kwa sababu malengo yanakuwa endelevu na mafanikio pia yanakuwa ni endelevu, unapanga malengo unayatimiza na kufanikiwa, kisha unapanga tena. Kigezo cha kupima mafanikio ni pale ninapokamilisha malengo niliyojiwekea angalau kwa sehemu fulani, hata kama kuna changamoto. Vyovyote vile maisha yatakavyokuwa ili mradi niko kwenye mwendo wa kupiga hatua nahesabu nimefanikiwa. – Enelisa Mbwile

Nikiwa na fedha zinazoniwezesha kukidhi matakwa yangu hata kama sifanyi kazi, kuwa na fedha kwa ajili ya kusaidia wenye uhitaji na kuboresha afya yangu na kupata hekima kwa

kuhudhuria warsha mbalimbali Dunia na kufanya utalii Dunia kwa ajili ya kupumzika na kujifunza tamaduni za watu mbalimbali ni Mahitaji ya msingi yanayonichochea nitafute fedha zaidi. – Ramadhani Samizi

Mafanikio kwangu ni kuwa huru kifikra, kuwa huru kiroho, na kuwa na furaha kwa kusaidia jamii kujikwamua na umasikini. – Stephano Mbungu

## KIMBIA MBIO ZAKO.

Rafiki, nimeshirikisha maana hizi za mafanikio kwa wote ili uweze kujionea kwamba pamoja na kuwa tunapata mafunzo pamoja na wote tunataka kufikia mafanikio makubwa, bado mafanikio yana maana tofauti kwa kila mmoja wetu.

Hivyo jua maana yako ya mafanikio na hiyo ndiyo ikuongoze kwenye kila hatua unayochukua kwenye maisha yako. Kazana kuwa bora zaidi na kupiga hatua zaidi kila siku.

Usijilinganishe au kushindana na wengine, maana ya mafanikio kwako siyo sawa na yao. Ushindi kwenye maisha yako siyo kuwazidi wengine, bali kufikia maana ya mafanikio kwako.

Lakini pia kuijua maana kabla hujafanikiwa inakusaidia kuridhika na mafanikio unayokuwa umeyapata.

Mafanikio hayana ukomo, kila unachopata, utaona unaweza kupata zaidi. Kama hujui maana ya mafanikio kwako, kila mara utakuwa huridhiki, utajiona hakuna ulichofanya kwa sababu kuna hatua zaidi za kupiga.

Lakini unapoijua maana ya mafanikio kwako, unaridhika kwa kuwa umeifikia, hata kama kuna hatua zaidi unazoweza kupiga, hujioni kama umeshindwa, bali unajiona umefanikiwa huku ukiwa na fursa za kufanikiwa zaidi.

Nikutakie kila la kheri katika kuijua, kuielewa na kuiishi maana yako ya mafanikio, hiyo ndiyo ramani kuu ya maisha yako.

# MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021